


# Kanuni za Msingi za Kilimo Bora cha zao la Muhogo Tanzania

AKILIMO
we know cassava

- **HATUA 1:** Kuchagua eneo
- **HATUA 2:** Kusafisha Shamba
- **HATUA 3:** Kunyunyizia kiuagugu
- **HATUA 4:** Kukatua na kuweka matuta
- **HATUA 5:** Kupanda
- **HATUA 6:** kudhibiti magugu

## HATUA 1: Kuchagua Eneo

Chagua eneo lenye udongo usio na mawe, kina kifupi, lisilotuama maji na lisilo na mteremko mkali. Uwepo wa Shughuli za viumbe hai (Minyoo na wadudu) ni dalili za udongo wenye rutuba.

## HATUA 2: Kusafisha Shamba

**Ni upi muonekano wa shamba lako?**













- **Uoto kidogo** → Shamba lako lina aina ya magugu haya?
- **Kichaka (Miti)** → Fyeka na safisha shamba. Ikibidi, Ondoa visiki. → Shamba lako lina aina ya magugu haya?
- **Majani Mapana** → Uoto ni mbichi na kijani.
  - LA → Fyeka na safisha shamba. Ikibidi, Ondoa visiki.
  - NDIO → Uoto ni mrefu kupita magoti (sm 50).
    - NDIO → Fyeka na safisha shamba. Ikibidi, Ondoa visiki.
    - LA → Nenda hatua 3
- **Nyasi** → Uoto ni mrefu kupita magoti (sm 50).
  - LA → Nenda hatua 3
  - NDIO → Fyeka, safisha na acha magugu yachipue kwa wiki 2. → Nenda hatua 3

Shamba lako lina aina ya magugu haya?



(Angalia maelezo kwenye karatasi nyingine)

- NDIO → Nenda hatua 3
- LA → Nenda hatua 4

## HATUA 3: Kunyunyiza Kiuagugu

Nyunyuzia kiuagugu chenye glyphosate kwa kiwango kilicho kwenye kibandiko (angalia orodha ya viuagugu kwenye karatasi nyingine). Subiri kwa wiki 2 ili mimea ife

Scanned with CamScanner

## HATUA 4: Kukatua na Kuweka Matuta

Kutayarisha shamba ni gharama. Kuwekeza katika kukatua na kuweka matuta lazima kulete faida inayotokana na ongezeko la mavuno. Kuwekeza kwenye kutayarisha shamba kunashauriwa endapo shamba litatuzwa vizuri, kufuata ushauri uliotolewa hatua ya 2 na 3 na kudhibiti magugu kwa wakati na kwa ufanisi. Shamba lako lazima liwe na rutuba ya kutosha ili kuweza kupata mavuno si chini ya tani 5 kwa ekari

Natarajia mavuno si chini ya tani 5 kw aekari

- NDIO → Kukatua kutaongeza mavuno yako kwa tani 2 au zaidi kwa ekari. Kokotoa faida unayotarajia :

  2 × Bei ya Muhogo (TZS kwa tani)

  Je faida hii ni kubwa kuliko gharama ya kukatua (TZS kwa ekari)?
  - NDIO → Katua shamba lako → Kuweka matuta
  - LA → Usikatue → Kuweka matuta
- LA → Usikatue → Ni vigumu kudhibiti magugu shambani kwangu AU Natarajia kuvuna Wakati wa kiangazi. AU Udongo wangu ni wa mfinyazi na unatuama maji
  - LA → Usiweke matuta
  - NDIO → Weka matuta

Kuweka matuta kutaongeza mavuno Kwa angalau tani 1.5 kwa ekari. Kokotoa faida unayotarajia:

1.5 × Bei ya Muhogo (TZS kwa tani)

Je faida ni kubwa kuliko gharama ya kukatua (TZS kwa ekari)?
- NDIO → Weka matuta
- LA → Ni vigumu kudhibiti magugu shambani kwangu AU Natarajia kuvuna Wakati wa kiangazi. AU Udongo wangu ni wa mfinyazi na unatuama maji

## HATUA 5: Kupanda na Kuzuia Magugu Kabla ya Kuota

1. **Panda muhogo kweye udongo wenye unyevu wa kutosha.**
   Nafasi iliyoshauriwa kupanda ni m1 kati ya mstari na mstari na m1 kati ya muhogo na muhogo (Au m1 x m0.9 kama unatarajia uchipuaji mdogo).

2. **Nyunyizia kiuagugu kinachopendekezwa ndani ya masaa 24 baada ya kupanda.**
   Usinyunyizie kiuagugu kwenye udongo mkavu.

3. **Tembelea shamba mara kwa mara.** Rudishia vipando ambavyo havikuchipua baada ya wiki 2-3

* Pata vipando visivyo na magonjwa kutoka kwa vyazo vilivyothibitshwa . Tembelea https://seedtracker.org/cassava/

## HATUA 6: Kudhibiti Magugu Baada ya Muhogo Kuota

1. Palilia kila uoto wa magugu unapofika 1/3 ya shamba na ukiwa na majani 4-6 .Nyunyizia kiuagugu cha baada ya kuota, tumia machine ya kupalilia, au palilia kwa kutumia jembe la mkono au panga.

2. Iwapo unanyunyizia kiuagugu cha baada ya kuota, kitumie sehemu ya shamba yenye magugu jamii ya nyasi

3. Iwapo shamba lina magugu yenye majani mapana, au mchanganyiko Wa majani mapana na nyasi, kiuagugu aina ya **glufosinate ammonium au glyphosate** Chaweza kutumiwa moja kwa moja kuua magugu chini ya mwanvuli wa mmea

4. **Usitumie glyphosate or glufosinate ammonium kwenye muhogo wenye umri chini ya wiki 8!** Iwapo muhogo una umri chini ya wiki 8 palilia kwa kutumia mashine au jembe la mkono kudhibiti magugu yenye majani mapana.

5. *Glyphosate au glufosinate ammonium* vyaweza kutumika Wiki 8 baada ya kupand a. **Tumia bomba lenye kizuizi kuepuka kiuagugu kugusa majani au shina la muhogo .**

6. **Badilisha aina ya viuagugu baada ya msimu kuzuia magugu kujenga usugu**

**Tahadhari: Kwa sababu za Kiafya, epuka kiuagugu chenye paraquat!!!**

IITA Transforming African Agriculture

TARI

AKILIMO TANZANIA ASSOCIATION

viamo

Watumiaji wa Vodacom Tanzania wanaweza kupata taarifa hii kwa kupiga namba 321

**WASILIANA NA :** akilimo@cgiar.org
AU tembelea tovuti yetu www.akilimo.org

Scanned with CamScanner